# DARASA LA SITA - 2020

# KISWAHILI: LUGHA

*Muda: Saa 1 Dakika 40*

***Soma kifungu kifuatavyo. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Siku ___1___ sikuenda ___2___. Nilikuwa ___3___ sana na kutapika. Baba na mama ___4___ walinichukua na kunipeleka ___5___ kumwona ___6___. Nesi ___7___ tumngoje amalize kumtibu mgonjwa mwingine. Nesi huyo ___8___ aliyenionyesha mahali ___9___ kukaa. Alikuwa mwaminifu kama ___10___. Nilipochunguzwa, niliambiwa kuwa ___11___ ugonjwa wa kipindupindu. ___12___ na kuanza kulia ___13___ uchungu. ___14___ wangu walinituliza na kunishauri niwe nikila chakula kisichokuwa na uchafu na kunywa maji ___15___.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. umoja | B. mmoja | C. kimoja | D. moja |
| **2.** | A. kwa shule | B. shule | C. shuleni | D. kwa shuleni |
| **3.** | A. nikiendesha | B. nikihara | C. nikiendeshwa | D. ninaendesa |
| **4.** | A. wangu | B. yangu | C. langu | D. zake |
| **5.** | A. shuleni | B. msalani | C. hospitalini | D. nyumbani |
| **6.** | A. seremala | B. topasi | C. bawabu | D. mganga |
| **7.** | A. aliniambia | B. alituambia | C. alikuambia | D. aliwaambia |
| **8.** | A. ndiye | B. ndio | C. ndiyo | D. ndiwo |
| **9.** | A. pa | B. mwa | C. ya | D. la |
| **10.** | A. mchana | B. malaika | C. mtoto | D. mzazi |
| **11.** | A. niligonjeka | B. niliugua | C. niliungua | D. nilingojeka |
| **12.** | A. Ninashangaa | B. Nilishanga | C. Ninashanga | D. Nilishangaa |
| **13.** | A. katika | B. kwenye | C. kwa | D. na |
| **14.** | A. Wasasi | B. Wazazi | C. Mzazi | D. Msasi |
| **15.** | A. chafu | B. masafi | C. safi | D. machafu |

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, chagua jawabu lifaalo zaidi.***

**16.** Chagua wingi wa:
**Mfuko huu ni wa dawa ya mtoto.**
A. Mifuko hii ni ya madawa ya watoto.
B. Mifuko haya ni ya dawa za watoto.
C. Mifuko haya ni ya madawa ya watoto.
D. Mifuko hii ni ya dawa za watoto.

**17.** Tumia kiulizi sahihi kujazia nafasi.
**Mwalimu _______ ambaye ananiita?**
A. mgani B. upi
C. yupi D. wagani

**18.** Chagua orodha ya nomino zinazopatikana katika ngeli ya **KU - KU**.
A. Kufuli, kuku, kuta.
B. Kunguru, kucha, kula.
C. Kuruka, kuku, kule.
D. Kutembea, kucheza, kulala.

**19.** Sentensi gani sahihi kati ya hizi?
A. Mvua umenyesha sana.
B. Chai ya maziwa yalinywewa na mtoto.
C. Makarai ya shangazi yamewekwa.
D. Magari zile zimebeba abiria.

20. Gani **si** kivumishi cha pekee kati ya hivi?
A. wengi B. vingine
C. yoyote D. lenyewe

21. Tumia jibu linalofaa kijazia kihasho.
**Mimi ____ mwalimu wenu wa Kiswahili.**
A. ndiye B. ndimi
C. ndio D. ndiwe

22. Chagua sentensi iliyotumia **'ki'** kuonyesha masharti?
A. Kitoto kile kinajua kuimba.
B. Vyakula vya kiasili vinasaidia afya.
C. Ukisoma kwa bidii utapita mtihani.
D. Mama alikuwa akipika nilipowasili.

23. Tambua kivumishi cha sifa katika sentensi ifuatayo.
**Mzee yule wenu amebeba chakula kizuri.**
A. chakula B. wenu
C. yule D. kizuri

24. Kitenzi **'peleka'** kitakuwaje katika hali ya kutendea?
A. pelekwa B. pelekea
C. pelekeka D. pelekesha

25. Kutokana na kitenzi **soma** tunapata nomino ____________
A. mwalimu B. mwanafunzi
C. somesha D. somo

26. Tambua kiungo cha mwili ambacho ni tofauti na vingine.
A. ulimi
B. kwapa
C. paja
D. wayo

27. Sentensi ipi ambayo **haijatumia** tanakali ya sauti iliyo sahihi?
A. Jiwe limeanguka majini chubwi!
B. Barabara hii imenyooka twaa!
C. Gunia lilianguka barabarani pu!
D. Sarafu ilianguka mchangani tang!

28. Mtu anaposafiri huhitajika kulipa _____
A. karo B. mahari
C. nauli D. koto

29. Barua rasmi huwa na anwani ngapi?
A. 1 B. 2
C. 3 D. 4

30. Sentensi ipi iliyotumia kiunganishi kwa usahihi?
A. Sikunywa chai wala sikula ugali.
B. Nilienda kwao na sikumpata.
C. Mtoto alianguka wala hakulia.
D. Amepewa zawadi lakini amepita mtihani.

<u>***Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 31 hadi 40.***</u>

Naliaka aliamka alfajiri kama ilivyokuwa desturi yake, saa **kumi na mbili** juu ya alama. Kabla ya kuoga, alipiga dua kisha akapiga meno mswaki. Kuoga kulifuatwa na kujipodoa kabla ya **kupiga miguu** kuelekea kwenye stani ya magari. Alishangaa sana kuona watu wengi wakitembea kuelekea kazini. Kikawaida wengi mno walitumia magari ya umma. Alipofika kwenye stani, hapo ndipo mshangao wa mwaka ulipompata. **Magari ya abiria yalikuwa wali wa duku**. Abiria walisongamana pale kama nzi kwenye mzoga.

Magari machache yaliyofika pale yalilipisha nauli mara mbili. Naliaka alikuwa na shilingi mia moja za nauli, hamsini za kumfikisha mjini na hamsini za kumrudisha. Abiria mmoja pale aliposimama alimfahamisha kuwa magari ambayo hayakuzingatia sheria za barabara yalipigwa marufuku. Magari yote ya umma yalilazimika kuwa na mikanda au mishipi ya usalama. Pia yalilazimika kuwa na vidhibitimwendo. Vidhibitimwendo vilifaa kuhakikisha kuwa magari hayaendeshwi kwa kasi ya kupita kilomita themanini kwa saa.

Naliaka alipigwa na butwaa kwa sababu sheria hizo hazikuwa mpya nchini. Alikumbuka kuwa sheria hizo zilikuwa zimeanzishwa karibu mwongo mmoja uliopita na aliyekuwa waziri wa usafiri, Hayati Michuki

Hali hiyo haikuwa mpya kwa Wakenya. Sheria nyingi mno zilikuwapo lakini hazikufuatwa. Naliaka alikumbuka watu walioaga dunia, mama yake mzazi akiwemo, kutokana na kuporomoka kwa nyumba. Sheria za ujenzi zilikuwapo, lakini ni wajenzi wachache mno waliozifuata. Nyumba zilijengwa bila mpango. Maeneo mengine hayakufaa kujengwa nyumba, lakini ungeona majengo ya ngorofa kadhaa. Majengo mengine yaliyengwa bila kutumia vifaa vinavyofaa. Aidha, urefu wa ghorofa zingine ulipita kiasi. Utafiti ulionyesha kuwa ufisadi ndio ulisababisha matatizo haya yote. Naliaka alitoka pale na kurudi ndani ya nyumba.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza, ilikuwa kawaida ya Naliaka kufanya nini?
A. Kuamka mapema.
B. Kunywa kiamshakinywa.
C. Kuamka saa kumi na mbili jioni.
D. Kuoga baada ya kujipodoa.

**32.** Jambo gani ambalo Naliaka alilifanya mwisho kati ya haya?
A. Kuamka B. Kujipodoa
C. Kuoga D. Kupiga mswaki

**33.** **'Kupiga miguu'** ndiko kufanya nini?
A. Kukimbia B. Kukaa
C. Kusafiri D. Kutembea

**34.** Ni nini kilichomshangaza Naliaka kwenye stani ya magari?
A. Magari ya abiria yalikuwa machache.
B. Abiria walikuwa wali wa daku.
C. Abiria hawakuwa kwenye stani.
D. Magari ya abiria yalikuwa mengi.

**35.** Naliaka alitarajia kulipa shilingi ngapi hadi mjini?
A. Shilingi mia mbili.
B. Shilingi mia tatu.
C. Shilingi hamsini.
D. Shilingi mia moja.

**36.** Magari gani ambayo yalikuwa yamepigwa marufuku?
A. Magari yote ya umma.
B. Magari ya abiria yasiyozingatia sheria za barabarani.
C. Magari ya umma yaliyokuwa na mikanda.
D. Magari ya umma yaliyofuata sheria za barabarani.

**37.** Kulingana na aya ya pili, nini kilichofaa kuhakikisha kuwa magari hayaendeshwi kwa kasi?
A. Dereva B. Mikanda
C. Magurudumu D. Vidhibitimwendo

**38.** Sheria za barabarani zilianzishwa;
A. na mwongo mmoja uliopita
B. na Naliaka
C. na Hayati Michuki
D. na waziri wa usalama Hayati Michuki.

**39.** Mama wa Naliaka aliaga dunia kutokana na
A. ajali ya barabarani
B. sheria za ujenzi
C. kuporomoka kwa nyumba
D. ajali ya moto

**40.** Kwa nini Naliaka alirudi nyumbani badala ya kusafiri?
A. Magari hayakuwapo.
B. Hakuwa na nauli.
C. Muda ulikuwa umeenda sana.
D. Hakuwa na nauli ya kutosha.

**_Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali 41 mpaka 50._**

Je, kwa nini wanafunzi huenda shuleni? Elimu ina manufaa gani katika maisha yetu? Umuhimu wa kwanza wa elimu ni kuondoa ujinga. Kuna tabia ambazo mtu akizifanya huonekana kuwa ni ujinga. Mfano wa tabia hizo ni kuongea ukiwa na chakula mdomoni. Mtu ambaye amesoma hutarajiwa kujiepusha na tabia za aina hiyo. Vilevile, tabia za mtu za jumla hubadilika anapokuwa shuleni. Mwanafunzi hufundishwa maneno ya nidhamu na heshima kama vile asante, tafadhali, samahani, pole na mengineyo.

Faida nyingine ni kuwa elimu hutusaidia kuajiriwa na kujiajiri. Ajira kama vile ualimu, udaktari, urubani, unahodha na nyinginezo hupatikana tu na watu ambao wamesoma. Watu kama hao ndio wenye ujuzi na maarifa ya kuzifanya kazi hizo. Hata hivyo, si lazima kuwa ukisoma unategemea kuajiriwa tu. Maarifa ambayo mtu hupata masomoni yanaweza kumsaidia kujiajiri kwa kufungua biashara. Kupitia biashara kama hizo, mtu huyo huweza kuwaajiri wenzake na hivyo kupunguza umaskini nchini.

Isitoshe, elimu husaidia kuleta umoja nchini. **Umoja huisaidia sana nchi yetu**. Katika shule, watu wa makabila mbalimbali hushirikiana ili kupata elimu. Wao husoma, huketi na kuchezea pamoja bila kujali makabila yao. Wazazi wa wanafunzi hao pia hushirikiana ili kuhakikisha kuwa watoto wao wanafaulu katika mtihani. Walimu nao huungana na kufanya kazi pamoja ili wawasaidie wanafunzi. Hali hii hufanya walimu, wazazi na wanafunzi **wapendane kama chanda na pete**.

Hatimaye, elimu hutusaidia kuimarisha afya. Wanafunzi wakiwa shuleni, wao hufundishwa lishe bora yenye aina tatu za vyakula. Pia wao hufundishwa umuhimu wa usafi wa mwili na mazingira. Hili husaidia kuwaepushia wanafunzi maradhi kama vile kipindupindu. Jambo hili nalo huhakikisha kuwa watu ambao **wanaaga dunia** wamepungua. Je, unajua faida gani nyingine za elimu?

**41.** Kulingana na aya ya kwanza, mtu akiongea akiwa na chakula mdomoni
A. huonekana kuwa ni mjinga
B. huambiwa kuwa ni mjinga
C. hujiita mjinga
D. hujifanya mjinga

**42.** Mtu ambaye amesoma anatarajiwa kufanya nini?
A. Kutoroka tabia za ujinga.
B. Kufanya tabia za ujinga.
C. Kujiepusha na tabia za ujinga.
D. Kuendeleza abia za ujinga.

**43.** Neno gani ambalo ni la heshima na nidhamu lakini halijatajwa katika ufahamu?
A. Simile B. Tafadhali
C. Asante D. Pole

**44.** Chagua jibu ambalo ni kweli kulingana na aya ya pili.
A. Ni lazima mtu aliyesoma aajiriwe.
B. Watu wote waliosoma hawana ajira.
C. Si lazima mtu aliyesoma aajiriwe.
D. Watu wote ambao hawajasoma wameajiriwa.

**45.** Kufungua biashara kuna faida gani nchini?
A. Hupunguza ufisadi.
B. Huongeza elimu.
C. Hupunguza umaskini.
D. Hupunguza ukabila.

**46.** **'Umoja husaidia sana nchi yetu'** Methali gani inayokubaliana na maneno hayo?
A. Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.
B. Polepole ndio mwendo.
C. Chelewachelewa utapata mwana si wako.
D. Umoja ni nguvu utengano ni udhaifu.

**47.** Kulingana na ufahamu, ni nini ambacho wanafunzi hawafanyi wakiwa pamoja?
A. Kulala B. Kusoma
C. Kuketi D. Kucheza

**48.** **'... wapendane kama chanda na pete'** ni mfano wa _______
A. methali B. tashbihi
C. istiara D. tanakali

**49.** Ufahamu unaeleza kuwa lishe bora ina aina ngapi za vyakula?
A. 2 B. 4
C. 3 D. 5

**50.** Maneno **'wanaaga dunia'** yana maana gani namna yalivyotumiwa katika ufahamu?
A. Wanaondoka.
B. Wanafariki.
C. Wanaenda.
D. Wanaikataa dunia.